



TANGAZO LA KAZI YA UFUNDI WA UJENZI WA UZIO WA KARAKANA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE.

Tarehe. 15/03/2023.

TANGAZO LIMERUDIWA KUTANGAZWA

Ofisi ya mkurugenzi mtendaji ya wilaya ya Nyang'hwale imepokea fedha kutoka CSR kwa ajili ya Ujenzi wa Uzio wa Karakana kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hivyo Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) inatoa mwaliko wa Nukuu za bei kutoka kwa Local Fundi, Vikundi mbalimbali vivilvyosajiliwa, au Kampuni za Ujenzi kuleta maombi yao kwa ajili ya **Kujenga Uzio wa Karakana** ya Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale.

Kazi zinazotegemewa kufanya kwenye ujenzi huo zimefanuliwa kwa kina kwenye BOQ za ufundi ambazo zinapatikana katika Ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa tisa na nusu siku za kazi.

Mwombaji ni lazima aambatanishe BOQ ya ufundi katika maombi yake ambapo BOQ hiyo ya ufundi inapatikana kwenye Ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi . Sifa za Mwombaji:

1. Mwombaji ni lazima awe mtanzania na mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea.
2. Mwombaji ni lazima awe na uzoefu wa katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya serikali.
3. Mwombaji ni lazima awe na uwezo wa kusoma ramani ya kihandisi na kuilewawa.
4. Mwombaji ni lazima awe na Akaunti benki ambapo malipo yake yatapitia kwenye akaunti hiyo.
5. Mwombaji awe na uwezo wa kulipa vibarua wake ambao atawaajiri kufanya kazi.
6. Mwombaji awe na uwezo wa kupokea na kutekeleza maelekezo ya kitaalamu yatakayokuwa yanatolewa na wataalamu wa ujenzi wakati wa ujenzi.
7. Mwombaji ni lazima aambatanishe BOQ ya ufundi iliyojazwa bei wakati anawasilisha maombi ya kazi hii.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi hii ni tarehe **25/03/2023** saa tano kamili Asubuhi na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo saa tano na nusu asubuhi katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi. Fundi au mwakilishi wake anaruhusiwa kuhudhuria siku ya Ufunguzi.

Maombi yote yawasilishwe Katika Ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi,Muda wa kuwasilisha maombi ni kuanzia saa 2:00 Asubui hadi 10:00 Jioni Siku za kazi

Hivyo,Local Fundi,Vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa, au Kampuni za Ujenzi wanaopenda kufanya kazi hii wafike katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi Wilaya Nyang'hwale kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana siku za kazi kwa ajili ya kuchukua Nyaraka za Manunuzi ili waweze kujaza bei kwa kazi ya Kujenga Uzio wa Karakana ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

Mwisho wa kuja kuchukua kotesheni na kurejesha itakuwa ni tarehe **25/03/2023** saa tano kamili asubuhi na ufunguzi utafanyika saa tano na nusu Asubuhi katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi



Husna T Chambo
Mkurugenzi mtendaji (w)
NYANG'HWALE.

MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
NYANG'HWALE